

## **KANISA LA AGANO JIPYA SIKU YAKE YA IBADA**

Yesu alifufuliwa toka kwa wafu Siku ya Kwanza ya juma. Katika lugha ya Paulo, akatangazwa kuwa mwana wa Mungu mwenye nguvu . . . kwa kufufuka toka kwa wafu, (Rum. 1:4). Ni siku hiyo ndiyo aliwatokea wanafunzi wake. Juma moja baadaye aliwatokea tena Siku ya Kwanza ya juma (Yoh. 20:1, 19, 26).

Kanisa lilianzishwa Siku ya Pentekoste, ambayo pia iliangukia Siku ya Kwanza ya juma - siku hamsini baada ya sikukuu ya Pasaka ambayo iliishia na Sabato, (Law. 23:15,16).

Sabato ya siku ya saba ilitolewa kwa Wayahudi kwa ajili ya kumbukumbu ya kuadhimisha kutolewa kwao toka utumwani misri, (Kum. 5:15). Kufufuka kwa Bwana wetu kunaadhimisha kuokolewa kwetu toka dhambini na kaburini. Imekuwa vema kwa hiyo Kanisa kuwa na mwanzo wake Siku ya Kwanza ya juma, na baada ya hapo Wakristo wakutane siku hiyo kwa kusudi la wazi la kumwabudu Mungu, katika kumbukumbu ya mateso na kifo cha Bwana Yesu Kristo, katika kuadhimisha chakula chake, ambacho sio tu kinatukumbusha kifo chake kwa ajili ya dhambi zetu kinatumkumbusha pia kuja kwake kwa mara ya pili, (1 Kor. 11:26), wakati ambao “wote walio makaburini wataisikia sauti yake nao watatoka,” (Yn. 5:28, 29).

Ingawa wakati mwingine tunamwona Paulo akiingia ndani ya masinagogi ya Wayahudi. Katika miji mbali mbali siku ya sabato ya Wayahudi, akiwashawishi waachane na taratibu zao za awali za kuabudu na kumgeukia Bwana Yesu Kristo. Lakini kwa upande wa Wakristo hatuwaoni wakikutana kwa lengo la ibada siku ya sabato ya Wayahudi. Bali daima Siku ya Kwanza ya juma, wakati wanafunzi walipokusanyika kumega mkate, Paulo alihubiri mbele yao, akiwa tayari kuondoka siku ya kesho yake, (Mdo. 20:7). Wakati wakristo wa awali wakiwa katika tendo la ibada walipokusanyika kwa wakati uliostahili (Siku ya Kwanza ya Juma) mtume Paulo anataja wazi kwamba kusudi la kukutana huko lilikuwa ni kumega mkate. Hivyo katika mikutano yao yote kwa ajili ya ibada “Siku ya Kwanza ya Juma” wanafunzi wa awali walishiriki Meza ya Bwana (Chakula cha Bwana).

Kama inaweza kudadisiwa kwamba Wakristo wa awali haikuwa lazima kukutana kila Siku ya Kwanza ya juma, tunapaswa kujikumbusha wakati wa kutolewa amri kumi, Waisraeli waliambiwa tu, “ikumbuke siku ya sabato uitakase,” Kut. 20:8. Mtu mmoja kambini yaelekea alijisikia kwamba kwa sababu Bwana hakusema wazi wazi “kila siku ya sabato” basi haikuwa lazima kuishika kila siku ya hiyo. Lakini alipovunja sabato moja tu kwa kwenda

kukusanya kuni alitupwiwa mawe hadi kufa, kama Mungu alivyoamwamuru Musa, (Hes. 15:32-36).

Mwandishi wa kitabu cha Matendo (20:7) kinaelezea kusudi la kukutana wanafunzi wa awali “Siku ya Kwanza ya juma” ilikuwa ni kumega mkate.

Katika, 1Kor. 16:1, 2, tunaona ilikuwa ni utaratibu wa kanisa la awali kukutana Siku ya Kwanza ya kila juma. Siku ambayo walipaswa kufanya changizo kwa ajili ya kazi ambayo Bwana aliliwekea Kanisa. Hivyo, Paulo aliandika, “Kuhusu changizo kwa ajili ya watakatifu, kama nilivyoyaamuru makanisa ya Galatia nanyi fanyeni hivyo hivyo. Siku ya Kwanza ya juma,” ambayo ndivyo katika lugha ya awali panavyoonyesha msisitizo.

Kamwe Siku ya Kwanza ya juma haikutajwa kama ni “Sabato ya wakristo.” Dhahiri haikusemwa kamwe kuwa ndiyo “Sabato” wakati wowote, wala kudokezwa hivyo katika tukio moja wapo. Zaidi ya yote kumbu kumbu zote zilizotaja kuhusu ibada ya wakristo zinaonyesha ilifanyika “Siku ya Kwanza ya juma.” Lakini kamwe siku ya saba, au abato ya Wayahudi. Katika kifo cha Kristo, sabato ambayo ilihusu kumbukumbu ya kuokolewa Wayahudi toka utumwani Misri, ilipoteza maana yake. Kwa kweli haikuwahi kuwa na umuhimu wo wote kwa wakristo, (Kol. 2:14-16).

Si sahihi kusema mfalme Constantine “aliibadili” sabato kuwa Siku ya Kwanza ya juma. Alichokifanya kilikuwa ni kuitambua rasmi siku ambayo wakristo walikuwa wamezoea kukutana kuabudu tangu kanisa lianze wakati sabato ya Wayahudi kamwe haikuwahi kuwa sehemu ya Sheria za Rumi, Warumi walitambua kuwa Wayahudi walizoea kuiadhimisha siku ya saba katika juma, na hawakukataza mpaka wakati taifa la Israeli lilipoharibiwa na hekalu lao kuteketezwa, na siku ikawa imepoteza umaarufu wake kwao.

Ingawa Wakristo hawaadhimishi Siku ya Kwanza ya juma kwa maana ile ile ambayo Wayahudi waliadhimisha sabato yao, lakini kwa sababu ya umuhimu wake, Wakristo wawe waaminifu (wote) katika ukusanyikaji wao katika siku hiyo ili kumwabudu Mungu. Kufanya kumbukumbu ya mateso na kifo cha Bwana wetu, wakati tukitazamia ujio wake wa mara ya pili.

Sisi rafiki zako wa  
Kanisa la Kristo:

[www.kanisalakristo.com](http://www.kanisalakristo.com)  
[www.kountzeheath.vox.com](http://www.kountzeheath.vox.com)

